

## SIUMWI MARA YA PILI

1. Sikhofii kutukanwa, nakhofia kutukana,  
Vitabuni imenenwa, watu hupata laana,  
Madhambi mengi huvunwa, kwa ringo na kujiona,  
Siwezi kuramba tena, sumu nalokoswa nayo.
2. Simu nalokoswa nayo, nendeje kuramba tena?  
Nifishwapo nayo hiyo, vipi nitaonekana!  
Kwa hiyo siku ambayo, wazishi wamekutana?  
Kwa hiyo sirambi tena, sumu nalokoswa nayo.
3. Miba nalotonwa mwando, ngozi yangu ikachana,  
Ikanitia uvundo, hatibiwa n'kapona,  
Siiwekei upendo, mshawasha nayo sina,  
Mimi siyendei tena, sumu nalokoswa nayo.
4. Shimo alongiya nyoka, dhahiri siyo kwa dhana,  
Yuangiya na kutoka, mwenzangu kagongwa jana,  
Katu sitajipeleka, kwa nguvu tutagombana,  
Kamwe sitaramba tena, sumu nalokoswa nayo.
5. Tendo lile la awali, tunguze hazitapona,  
Ungeomba tafadhali, chombezo kila aina,  
Ninaswe mara ya pili, hola! Sitapatikana,  
Elewa sirambi tena, sumu nalokoswa nayo.
6. Hata shamba kwa kilimo, nitalima kwa namna,  
Shamba lisilo na chumo, kulima sitang'ang'ana,  
Nitaridhia kihamo, ndaa isijenitona,  
Ndomana sirambi tena, sumu nalokoswayo.
7. Nifugeje kwa shauku, ng'ombe wasiyozaana!  
Bora nitafuga kuku, nichinje na kutafuna,  
Katu sifugi chiriku, kidege nyama hakina,  
Nyimboze ni kutukana, ndo sumu ya ndege huyo.
8. Kuishi naye mwerevu, yataka busra pana,  
Bali mtu mpumbavu, jibwakoko alingana,  
Litupie nyama mbovu, hula kama ilonona,  
Tama hamu sina, sumu nalokoswa - nayo.

*Amiri A.S. Andanenga (Sauti ya Kiza)*  
*Kinondoni-Shamba*  
*DAR ES SALAAM, Tanzania.*